**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA**

BRELA

BUSINESS REGISTRATIONS AND LICENSING AGENCY

**WAKALA WA USAJILI WA BIASHARA NA LESENI**

# MASWALI YANAYOULIZWA MARA KWA MARA KUHUSU HUDUMA ZITOLEWAZO NA WAKALA WA USAJILI WA BIASHARA NA LESENI (BRELA)

## NENO LA AFISA MTENDAJI MKUU

Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), imeandaa kitabu hiki kwa ajili ya kujibu maswali ambayo yamekuwa yakiulizwa mara kwa mara na wadau wetu. Lengo likiwa ni kuongeza uelewa kwa wateja wetu kuhusu huduma tunazotoa na kuwawezesha kuzifikia kwa urahisi wakiwa popote.

Ahadi yetu kwa wadau wetu siku zote ni kuwapatia huduma bora na kwa wakati. Kitabu hiki ni sehemu ya jitihada za kutengeneza mazingira rafiki kwa wadau wetu ili waweze kupata huduma kwa urahisi na kwa kuzingatia Sheria, Kanuni, Miongozo na Taratibu zilizopo.

Ndani ya kitabu hiki, wadau wetu watapata majibu ya maswali yote ambayo yamekuwa yakiulizwa kuhusu vigezo na taratibu za kufanya usajili wa biashara, usajili au Leseni za Viwanda pamoja na huduma za baada ya usajili au kupata Leseni ili yawe mwongozo kwa wadau wetu katika kupata huduma yoyote wanayohitaji.

BRELA itaendelea kupokea maoni na mapendekezo ya kuboresha kitabu hiki kutoka kwa wadau mbalimbali ili kuweza kufikia kiwango cha matarajio yao. Vilevile tunatarajia ktabu kitaweza kutoa majibu ambayo yataweza kuwasaidia katika kuandaa maombi kwa njia ya mtandao na kuweza kuwasilisha kwa wakati.

Ni imani yangu kwamba, kwa kupitia kitabu hiki, malalamiko kuhusu changamoto mbalimbali ambazo zimekuwa zikijitokeza wakati wa kuandaa na kutuma maombi ya huduma mbalimbali yatapungua, na kuwa chachu ya Wadau wengi zaidi kupata huduma za BRELA.

**Nyaisa, G.S.**
**AFISA MTENDAJI MKUU**
**WAKALA WA USAJILI WA BIASHARA NA LESENI (BRELA)**

## DIBAJI

Wakala wa Usajili Wa Biashara na Leseni (BRELA) ilianzishwa chini ya Sheria ya Wakala za Serikali Na. 30 ya mwaka 1997 na kuzinduliwa rasmi tarehe 03 Disemba, 1999 chini ya Wizara ya Viwanda na Biashara. Jukumu la msingi la BRELA ni kusimamia shughuli za kibiashara nchini kwa kuzingatia sheria na kanuni zilizopo kwa lengo la kuweka mazingira mazuri ya kibiashara.

Uwekaji wa mazingira mazuri ya kibiashara unahusisha upatikanaji wa taarifa muhimu kwa Wadau kuhusu huduma zinazotolewa. Ndani ya kitabu hiki kuna majibu ya maswali yanayoulizwa mara kwa mara kuhusu huduma zinazotolewa na BRELA, ambayo yatawezesha kuwa na uelewa kuhusu huduma inayohitajika na namna ya kupata huduma hiyo.

Kitabu hiki kimegawanyika katika sehemu nne; ambazo zina maswali na majibu kuhusu Usajili wa Kampuni, Majina ya Biashara, miliki Bunifu (ambayo imegawanyika katika sehemu mbili Usajili wa Alama za Biashara na Huduma na kupata Hataza). na Leseni ambayo imegawanyika katika sehemu mbili; Leseni za Biashara za Kundi “A” na Leseni za Viwanda.

## SEHEMU YA KWANZA

## MASWALI NA MAJIBU KUHUSU HUDUMA ZA KAMPUNI
## A. IDARA YA MAKAMPUNI NA MAJINA YA BIASHARA

### I. USAJILI WA KAMPUNI

**1. Je, ni vitu gani muhimu vya kuzingatia kabla ya kuanza usajili wa Kampuni?**

Ili kuanza hatua za usajili wa Kampuni wahusika wanatakiwa kuwa na vitu vifuatavyo:-

a) Namba ya Kitambulisho cha Taifa inayotolewa na Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA) kwa watanzania, au nakala ya Hati ya kusafiria kwa raia wa kigeni (Passport),
b) Anuani ya barua pepe kwa wahusika wote (email addresses),
c) Namba za simu za kiganjani za wahusika,
d) Jina la Kampuni,
e) Anuani ya makazi/ofisi,
f) Katiba ya kampuni (Memorandum and Articles of Association).

**2. Ni njia gani inayotumika kufanya sajili mbalimbali BRELA?**

Usajili unafanyika kwa njia ya mtandao kupitia Mfumo wa Usajili kwa njia ya Mtandao unaoitwa Online Registration System (ORS). Wakati wa kufanya Usajili, wahusika wahakikishe wanakuwa na vitu vifuatavyo:-

a) Namba ya Kitambulisho cha Taifa inayotolewa na Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA) kwa watanzania au Hati ya Kusafiria kwa raia wa kigeni (Passport),
b) Barua pepe kwa wahusika (email addresses) na taarifa za anuani za makazi kwa wahusika na za ofisi,
c) Namba za simu za kiganjani za wahusika ambao ni wanahisa na wakurugenzi,
d) Jina la Kampuni linalopendekezwa,

e) Katiba ya Kampuni (Memorandum and Articles of Association).

**3. Je, kuna aina ngapi za Kampuni?**

Kuna aina tatu za Kampuni ambazo ni:-

a) Kampuni binafsi,
b) Kampuni za umma,
c) Kampuni za kigeni

**4. Hatua zipi za kufuata ili kukamilisha Usajili wa Kampuni kwa njia ya Mtandao (ORS)?**

a) Tembelea mfumo wa usajili kupitia https://ors.brela.go.tz au kupitia tovuti ya BRELA www.brela.go.tz na bofya LIMITED COMPANY ONLINE REGISTRATION,
b) Kama huna akaunti kwenye mfumo, bofya “huduma mtandao kwa watumiaji wasiosajiliwa, Ingia kwenye mfumo kwa kuweka jina la mtumiaji na neno la siri (nywila),
c) Bofya “anza” kisha chagua “huduma mtandao”,
d) Chagua kampuni,
e) Kwenye aina ya huduma chagua usajili wa kampuni mpya, kisha bofya endelea,
f) Kwenye aina ya kampuni, chagua aina ya kampuni, mfano Kampuni binafsi kisha bofya Endelea,
g) Kwenye fomu ya maombi, jaza taarifa zote zinazotakiwa ambazo zimewekwa alama ya nyota nyekundu (*),
h) Kumbuka kubofya kitufe cha “Hifadhi” kwa kila taarifa unayoingiza ili zisipotee,
i) Sehemu ya Mwombaji, jaza kauli ya uwakilishi kama ni Mkurugenzi/Katibu/Mwakilishi,
j) Kama mwombaji anaweza kubadili taarifa kwenye Mfumo wa ORS, bofya “anaweza kurekebisha taarifa ORS”,
k) Jaza taarifa za Kampuni kama Jina la Kmapuni, accounting

date na kasha utajaza namba ya uhifadhi wa Jina la Kampuni kamatu ulifanya hiyo huduma kabla ya kuanza kazi ya usajili na kama hukufanya hutajaza kitu.

l) Jaza taarifa zote kwenye sehemu ya ofisi ya kusajiliwa.

m) Kwenye sehemu ya shughuli ya kibiashara, bofya “Ongeza”, kisha jaza taarifa za wakurugenzi wa kampuni angalau wawili,

n) Sehemu ya Wakurugenzi, bofya Ongeza, kisha jaza taarifa za wakurugenzi wa kampuni angalau wawili.

o) Sehemu ya Katibu wa Kampuni, jaza taarifa za Katibu wa Kampuni.

p) Sehemu ya Mtaji wa Kampuni, chagua aina ya mtaji wa kampuni kama ni “Kawaida au Mwingine”.

q) Sehemu ya Hisa za mtaji zilizotolewa, weka Idadi ya Hisa zilizotolewa na thamani ya kila hisa,

r) Sehemu ya Wanahisa bofya Ongeza na ingiza taarifa za wanahisa wasiopungua wawili,

s) Sehemu ya idadi ya hisa zilizoshikiliwa, chagua mwana hisa kutoka kwenye orodha sehemu ya chagua mwanahisa kutoka orodha na Daraja kisha Bofya add shareholders to the table below,

t) Sehemu ya wawakilishi, weka taarifa za watu wanaoweza kufanya marekebisho au mabadiliko kwenye mfumo wa ORS. Kama Wakurugenzi / wanahisa wanaweza kufanya marekebisho, bofya anaweza kurekebisha taarifa kwenye mfumo wa ORS, kisha bonyeza kitufe cha Endelea.

u) Mfumo utakupeleka sehemu ya kupakua na kupakia fomu na malengo na katiba ya kampuni. Subiri fomu ya majumuisho (Consolidated form) kisha ipakue, weka saini na tarehe na scan fomu hiyo,

v) Pakua fomu ya maadili, saini na gonga muhuri wa kampuni.

w) Pakia fomu ya majumuisho (consolidated form), fomu ya maadili (Integrity form), malengo ya katiba ya kampuni (Memorandum and Articles of Association) kisha bofya Endelea,

x) Mfumo utakupeleka kwenye ukurasa wa kufanya malipo na chagua njia unayotaka kufanya malipo,

y) Pakua taarifa ya maelekezo ya namna ya kufanya malipo na kisha fuata maelezo.

z) Baada ya kufanya malipo, maombi yako yatatumwa kwenye mfumo kwa ajili ya kufanyiwa kazi BRELA na yatahama kutoka sehemu ya Orodha yangu kwenda sehemu ya Maombi.

**5. Ni viambatisho gani ambavyo vitahitajika kwa ajili ya kukamilisha usajili wa Kampuni?**

a) Katiba ya Kampuni,
b) Fomu namba 14a (Consolidated form),
c) Fomu ya maadili (integrity form),
d) Nakala ya hati ya kusafiria kwa wasio raia wa Tanzania, na
e) Nyaraka nyingine ambazo msajili ana mamlaka ya kuziomba anapoona inafaa.

**6. Je, usajili wa kampuni unagharimu kiasi gani?**

**Ada ya usajili wa Kampuni inategemea na mtaji wa Kampuni kama ilivyoandikwa katika Katiba ya Kampuni na gharama zake ni kama ifuatavyo:-**

a) Mtaji unaozidi TZS 20,000/= na usiozidi TZS 1,000,000/= ada ni TZS 95,000/=
b) Mtaji unaozidi TZS 1,000,000/= na usiozidi TZS 5,000,000/= ada ni TZS 175,000/=
c) Mtaji unaozidi TZS 5,000,000/= na usiozidi TZS 20,000,000/= ada ni TZS 260,000/=
d) Mtaji unaozidi TZS 20,000,000/= na usiozidi TZS 50,000,000/= ada niTZS 290,000 /=
e) Mtaji unaozidi TZS 50,000,000/= ada ni TZS 440,000 /=

**7. Nawezaje kulipa ada ya usajili wa Kampuni baada ya kuingiza taarifa katika mfumo wa usajili wa ORS?**

Baada ya kukamaliza kujaza taarifa katika mfumo, utatengeneza namba ya malipo kupitia Mfumo wa Malipo ya Serikali (GePG). Baada ya kupata namba ya malipo, unaweza kufanya malipo kupitia mitandao ya simu au benki.

**8. Je inachukua muda gani maombi kukamilika na kupata cheti?**

Endapo taarifa zilizoingizwa katika mfumo zitakuwa sahihi kwa mujibu wa sheria, cheti hutolewa kwa njia ya mfumo ndani ya siku tatu na ikiwa taarifa za ziada zitahitajika pia ndani ya siku tatu mwombaji atakuwa amejulishwa ili kufanya marekebisho au nyongeza ya taarifa.

**9. Je, ni namna gani naweza kupata cheti cha usajili wa Kampuni?**

Baada ya maombi kupitishwa na msajili, cheti cha usajili hutolewa kupitia mfumo wa ORS katika akaunti iliyotumika kuwasilisha maombi ya usajili sehemu ya maombi (application)

**10. Je, Kampuni hufanya malipo ya kuwasilisha taarifa ya mwaka kila baada ya muda gani?**

Kila baada ya miezi 12 baada ya kampuni kusajiliwa

**11. Ninawezaje kuwasilisha taarifa ya mwaka ya Kampuni?**

Kwa kujaza fomu Na. 128 inayopatikana katika mfumo wa ORS na kuwasilisha kupitia mfumo. Fomu hii hujazwa kila mwaka tareheileile iliyosajiliwa Kampuni

**12. Nini hutokea pindi Kampuni inapochelewa kuwasilisha taarifa ya mizania ya mwaka kwa wakati?**

Kampuni ikichelewa kuwasilisha taarifa ya mizania ya mwaka kwa wakati italazimika kulipa ada ya kuchelewa kuwasilisha kiasi cha TZS 2,500/= kwa kila mwezi ilizochelewa. Kampuni inapochelewa kuwasilisha taarifa hizi kwa wakati inakuwa katika hatari ya kufutwa na Msajili wa Makampuni kwa mujibu wa sheria.

**13. Je, hatua zipi za kufuata ili kufanya mabadiliko mbalimbali ya Kampuni?**

Kuna hatua mbalimbali za kusajili wakati wa kufanya mabadiliko kwenye Kampuni. Mfumo wa ORS unampatia mteja uhuru wa kuchagua mabadiliko anayotaka kuyafanya kwa kuingiza taarifa za mabadiliko husika.

**14. Ninawezaje Kuhuisha taarifa za kampuni kupitia Mfumo wa Usajili wa kwa njia ya Mtandao (ORS)?**

Kwa kufungua akaunti katika Mfumo wa ORS na kuingiza taarifa za Kampuni zifuatazo:-

a) Jina la Kampuni, anwani ya Kampuni,
b) Namba za vitambulisho vya Taifa vya Wakurugenzi na Wanahisa,
c) Namba za utambulisho wa mlipa kodi (TIN),
d) Anwani ya makazi ya Wakurugenzi na Katibu wa Kampuni,
e) Namba za simu za Wakurugenzi na Wanahisa,
f) Mtaji wa Kampuni na mgawanyo wa hisa kwa kila mwanahisa kwa Kampuni yenye mtaji.

**15. Je, ninawezaje kupata taarifa za Kampuni iliyosajiliwa?**

Kwa kuomba kupitia Mfumo wa ORS (kwa kulipia kati ya 22,000/= hadi 30,000/= kulingana na aina ya nyaraka) au kutembelea Ofisi za BRELA ambapo mteja atalipia Ada ya kupekua jalada kiasi cha TZS 3,000 na atapatiwa jalada husika ili aweze kupekua moja kwa moja.

**16. Je, Kampuni inaweza kufungwa kwa utaratibu upi?**

**Kampuni inaweza kufungwa kwa njia mbili:-**

a) Kwa hiari ya wamiliki wa Kampuni au
b) Kwa amri ya Mahakama.

**17. Kampuni inayofungwa kwa hiari ya wamiliki wa Kampuni hufuata hatua zifuatazo:-**

a) Kwa kukaa kikao cha wanahisa na kupitisha Azimio la kufunga Kampuni husika,
b) Kutangaza Azimio katika Gazeti la Serikali na Gazeti la kawaida linalotoka kila siku,
c) Kupata cheti cha uthibitisho kutoka Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kuwa Kampuni haidaiwi Kodi ya Serikali na
d) Kuwasilisha taarifa ya mwaka endapo Kampuni haijawasilisha.

**18. Je, ninaweza kuhifadhi jina la Kampuni?**

Unaweza kuhifadhi jina la Kampuni kwa kutuma maombi ya jina linalopendekezwa kupitia kwenye mfumo wa ORS na baada ya jina kukubaliwa huweza kuhifadhiwa kwa siku 60 kwa kulipia ada ya uhifadhi wa jina kwa kiasi cha TZS 50,000/=.

## II. MMILIKI MANUFAA WA KAMPUNI
## WAKALA WA USAJILI WA BIASHARA NA LESENI (BRELA)
## KIPEPERUSHI KUHUSU WAMILIKI MANUFAA

### 1. Nini Maana ya Mmiliki Manufaa?

Mmiliki Manufaa (Beneficial owner) ni mtu ambaye anamiliki moja kwa moja au kwa kupitia mtu mwingine, zaidi ya asilimia 5% ya uwekezaji au ufanyaji maamuzi kwenye kampuni.

### 2. Je, ni Wamiliki Manufaa wapi wanaopaswa kuwasilisha taarifa zao kwa Msajili?

**Wamiliki manufaa wanaotakiwa kuwasilisha taarifa zao kwa Msajili ni wale ambao;-**

a) Wanaomiliki hisa katika kampuni kuanzia 5% au Zaidi.
b) Wenye idadi kubwa ya kura katika kufanya maamuzi ya kampuni, mamlaka ya kuchagua, au kuondoa sehemu kubwa ya wakurugenzi katika bodi ya kampuni.
c) Wenye ushawishi mkubwa au uamuzi wa mwisho kwenye kampuni.
d) Wenye makubaliano kati ya wanahisa au wanachama wenyewe kupitia mahusiano ya kifamilia au mahusiano mengine na watoa maamuzi.

### 3. Umuhimu wa taarifa za Mmiliki Manufaa

a) Kuongeza uwazi, uaminifu na uwajibikaji
b) Kuboresha mazingira ya uwekezaji
c) Kupunguza vitendo vya uhalifu wa kifedha vyenye kuathiri jamii.
d) Kuboresha utawala wa sheria

**4. Taarifa zipi zinazotakiwa kuwasilishwa kwa Msajili?**

a) Taarifa binafsi za Wamiliki Manufaa mf. Jina, anuwani, makazi n.k
b) Taarifa za kukoma kwa Ummiliki Manufaa.
c) Taarifa za mabadiliko ya wamiliki manufaa.

**5. Nani, anawajibika kuwasilisha taarifa za Mmiliki Manufaa kwa Msajili?**

Wakurugenzi au Katibu wa Kampuni.

**6. Je, Daftari la Wanachama na Wamiliki Manufaa ni nini?**

Ni daftari lenye taarifa za Wanachama na Wamiliki Manufaa linalotunzwa na kuhuishwa na kampuni yenyewe.

**7. Je, Daftari la Wamiliki Manufaa**

Ni daftari lenye taarifa za Wamiliki Manufaa wa Makampuni linalotunzwa na kuhuishwa na Msajili wa Makampuni.

**8. Utaratibu wa Uwasilishaji wa taarifa za Mmiliki Manufaa kwa Msajili.**

| | **Fomu** | **Muda wa kuwasilisha Taarifa** |
|---|---|---|
| **Uwasilishaji wa taarifa za Wamiliki Manufaa** | 14b | Makampuni yaliyokwishasajiliwa - kabla ya tarehe 01 Julai 2022.<br><br>Makampuni mapya – Ndani ya **siku 30** baada ya kusajiliwa. |

| | | |
|---|---|---|
| **Utoaji wa taarifa kipindi ambacho Mmiliki Manufaa atafikia ukomo** | 14c | Ndani ya **siku 30** baada ya Mmiliki Manufaa kufikia ukomo. |
| **Utoaji wa taarifa ya mabadiliko ya Mmiliki Manufaa.** | 14f | Ndani ya **siku 30** baada ya mabadiliko ya taarifa za Mmiliki Manufaa kufanyika. |

**9. Je, nani anaweza kupata taarifa za Wamiliki Manufaa?**

Taarifa za Wamiliki Manufaa ni taarifa za siri ambazo kwa mujibu wa sheria, hutolewa kwa Mamlaka Zilizoidhinishwa kama vile TRA, PCCB, FIU, Polisi n.k

**10. Je makampuni yenye ukomo wa ahadi yanatakiwa kuwasilisha taarifa za Wamiliki Manufaa?**

Ndio. Kwakuwa makampuni yenye ukomo wa ahadi hayana muundo wa hisa, hivyo basi, wanachama wenye ushawishi katika kufanya maamuzi, au wanaomiliki maslahi makubwa, au wenye mamlaka ya kuteua au kuondoa viongozi waandamizi katika uongozi watachukuliwa kama Wamiliki Manufaa.

**11. Je, nini kifanyike kama kampuni imeshindwa kuwatambua Wamiliki Manufaa wake?**

Pale jitihada zote za kuwatambua Wamiliki Manufaa katika Kampuni zinaposhindikana, basi, viongozi waandamizi wa Kampuni (Wakurugenzi au Afisa Mtendaji Mkuu)watachukuliwa kama ndio Wamiliki Manufaa. Makampuni yaliyoshindwa kuwasilisha taarifa za Wamiliki Manufaa yatapaswa kutunza taarifa za jitihada zilizofanyika kutambua Wamiliki Manufaa wake.

**12. Je, athari za kuchelewa kuwasilisha taarifa za Wamiliki Manufaa kwa Msajili ni zipi?**

Kampuni ikichelewa kuwasilisha taarifa za Wamiliki Manufaa kwa wakati, itawajibika kulipa ada ya ucheleweshaji kiasi cha Shilingi Elfu Mbili mia tano (TZS 2, 500) kwa mwezi.

**13. Je, athari za kutokuwasilisha taarifa za Wamiliki Manufaa kwa Msajili ni zipi?**

Kampuni itakapokutwa na hatia ya kutowasilisha, kutotunza, kutotoa taarifa za mabadiliko, au kutoa taarifa za uongo kuhusu Wamiliki Manufaa, itawajibika kulipa faini isiyopungua shilingi Milioni Tano (TZS 5,000,000) lakini isiyozidi Shilingi Milioni kumi (TZS 10,000,0000).

**14. Je, gharama za Uwasilishaji wa Taarifa za Wamilki Manufaa ni zipi?**

Gharama za uwasilishaji taarifa za Wamiliki Manufaa ni Shilingi za Elfu Ishirini na Mbili (TZS 22,000) kwa kila fomu moja itakayowasilishwa.

**15. Je akaunti ya ORS inaweza kutumika kuwasilisha taarifa za Wamiliki Manufaa?**

Kwa sasa, mfumo wa uwasilishaji taarifa za Wamiliki Manufaa ni mfumo unaojitegemea kutoka kwenye mfumo wa Usajili kwa Njia ya Mtandao (ORS). Hivyo mkurugenzi au katibu wa kampuni atapaswa kutengeneza akaunti mpya kwa ajili ya kuingia na kuwasilisha taarifa hizo kwenye mfumo wa Wamiliki Wanufaika.

**16. Nini kifanyike endapo Mmiliki Manufaa kwenye Kampuni ni Serikali?**

Kampuni itapaswa kumwandikia Msajili barua ya kutoa taarifa

ikiambatanishwa na kielelezo kuthibitisha kwamba Kampuni hiyo inamilikiwa na Serikali, kama vile Amri ya kuanzisha Taasisi hiyo (Establishment Order).

**17. Je, mtu ambaye ana maombi yanayoendelea kushughulikiwa kwenye mfumo wa Online Registration System (ORS) anaweza kuwasilisha taarifa za Wamiliki Manufaa?**

Ndiyo. Mfumo wa kupokea taarifa za Wamiliki Manufaa ni mfumo unaojitegemea kutoka kwenye mfumo wa Online Registration System (ORS) hivyo kampuni ambazo zina maombi yanayoendelea kwenye ORS bado zinaweza kuwasilisha taarifa zake za Wamiliki Manufaa kupitia https://bo.brela.go.tz.

**18. Je ni utaratibu gani unatumika kuwasilisha Taarifa za Wamiliki Manufaa ambao ni Watu Mashuhuri?**

Mtu Mashuhuri ni mtu ambaye amekasimishwa madaraka ya juu ya uongozi katika Serikali, Jeshi, Mahakama, viongozi waandamizi wa Siasa, na viongozi wakuu wa Taasisi za Serikali na Mashirika ya Umma ndani na nje ya nchi. Makampuni ambayo Wamiliki Manufaa wake ni Watu Mashuhuri, wanawajibu wa kuwasilisha taarifa za Wamiliki Manufaa hao zikiambatishwa na kiapo cha kuthibitisha kuwa Wamiliki hao ni watu Mashuhuri.

**19. Je, kampuni inapaswa kuwasilisha taarifa za Wamiliki Manufaa kwa Msajili kila baada ya muda gani?**

Taarifa za Wamiliki Manufaa zinawasilishwa mara moja tu. Aidha, endapo kutatokea mabadiliko yoyote kuhusu Wamiliki Manufaa, Kampuni itapaswa kuwasilisha mabadiliko hayo kwa Msajili ndani ya siku 30.

**20. Je, matawi ya makampuni ya kigeni yanawajibu wa kuwasilisha taarifa za Wamiliki Manufaa kwa Msajili?**

Hapana. Tawi la kampuni ya kigeni halina wajibu wa kuwasilisha taarifa za Wamiliki Manufaa kwa Msajili.

**21. Kama Wanahisa wanaoonekana kwenya nyaraka za usajili wa kampuni ndio hao hao Wamiliki Manufaa, je, kampuni bado ina wajibu wa kuwasilisha taarifa zao kwa Msajili?**

Ndio. Mwanahisa ambaye pia ni Mmiliki Manufaa wa Kampuni bado ana wajibu wa kuwasilisha taarifa zake kama Mmiliki Manufaa kwa Msajili.

## SEHEMU YA PILI

## MASWALI NA MAJIBU KUHUSU HUDUMA YA USAJILI WA MAJINA YA BIASHARA

**1. Ni taratibu zipi za kufuata ili kusajili Jina la Biashara?**

Kwanza utatakiwa kufungua Akaunti kwenye mfumo wa usajili kwa njia ya mtandao uitwao Online Registration System (ORS) na kuingiza taarifa za Jina la Biashara.

**2. Ni vitu gani ambavyo vinaweza kuniwezesha kumiliki Jina la Biashara?**

Kwanza unatakiwa kuchagua jina litakalotumika katika biashara yako na kusajili ikiwa jina unalotumia kwenye biashara yako halijafanana/sajiliwa na mtu mwingine basi utasajili na kumiliki jina husika katika biashara yako. Ikiwa jina la biashara limefanana na jina lingine lililosajiliwa na linatumika kwa biashara nyingine basi utatakiwa kubadili jina hilo.

**3. Ni taarifa zipi ambazo zitanilazimu kujaza katika Mfumo wa Usajili wa ORS pindi ninaposajili Jina la Biashara?**

Mfanyabiashara atatakiwa kujaza taarifa za umiliki kwa kutumia kitambulisho cha Taifa (NIDA) kinachotolewa na Mamlaka ya Vitambulisho, anwani ya Barua Pepe, namba za simu, anwani ya sanduku la barua, anwani ya eneo la biashara, anwani ya makazi ya biashara na aina ya biashara inayofanywa.

**4. Je, ni gharama kiasi gani inahitajika ili kukamilisha usajili wa Jina la Biashara**

Ada ya Usajili wa Jina la Biashara ni TZS 20,000/= tu

**5. Usajili wa Jina la Biashara unachukua muda gani kujibiwa baada ya kuwasilisha maombi?**

Inachukua muda usiozidi siku mbili ili kupata cheti cha usajili wa Jina la Biashara ikiwa taarifa zilizowasilishwa kwa ajili ya usajili wa Jina la Biashara zipo sahihi, na ikiwa kuna marekebisho basi mteja atakuwa amepata taarifa ndani ya siku mbili ili kufanya marekebisho husika.

**6. Je, nitajuaje kama maombi yangu yameshafanyiwa kazi?**

Utapata taarifa kupitia anuani ya barua pepe iliyowekwa katika akaunti ya mhusika katika mfumo wa ORS.

**7. Ni namna gani nitaweza kupata cheti changu cha usajili wa Jina la Biashara baada ya maombi kukamilika?**

Utapata cheti cha usajili kupitia kwenye akaunti iliyotumika kuingiza taarifa wakati wa usajili wa jina la biashara.

**8. Je, ninawezaje kufanya mabadiliko ya Jina la Biashara?**

Ikiwa unataka kufanya mabadiliko ya jina la biashara, utatakiwa kuingia kwenye mfumo uliotumika kusajili kwa kuingiza taarifa za mabadiliko husika na kujaza fomu Na.6

**9. Baada ya kupata cheti cha Jina la Biashara, ni muda gani natakiwa kufanya malipo ya utunzaji wa Jina la Biashara?**

Malipo ya utunzaji wa Jina la Biashara (Maintenance fee) yanafanyika kila mwaka. Ada ya mwaka ni TZS 5,000/=

**10. Je, nikichelewa kufanya malipo ya mwaka kwa wakati kuna faini yoyote ambayo nitatozwa siku ambayo nitakuwa nafanya malipo?**

Hakuna faini ya kuchelewa kufanya malipo ya mwaka isipokuwa

mhusika atatakiwa kulipia miaka yote ambayo hakufanya malipo.

**11. Ni kitu gani naweza kufanya ili nisirudishwe na marekebisho ya mfanano wa Majina?**

Kufanya utafiti kwa kupitia mfumo wa ORS uliowekwa kwa ajili kufanya ukaguzi wa majina kwa kuangalia asilimia (%) ya mfanano wa majina.

**12. Ni mfanano wa asilimia ngapi ambao unashauriwa baada ya kufanya utafiti wa Jina?**

Chini ya asilimia 50

**13. Je, ni vitu gani vinavyozingatiwa katika mfanano wa Majina ya Biashara?**

a) Kama yanafanana neno kwa neno,
b) kufanana kwa karibu,
c) Kufanana kwa matamshi mfano skuli na School,
d) Kufanana kwa muonekano na
e) Kufanana kwa tafsiri Kiswahili / Kiingereza.

**14. Ni namna gani naweza kubadili Jina la Biashara na kuwa Kampuni?**

Unaweza kubadili jina la biashara na kuwa Kampuni kwa kuanza na utaratibu wa kulifunga jina la Biashara na kisha kuandaa nyaraka kwa ajili ya usajili wa kampuni kwa kutumia jina lililokuwa linatumika.

**15. Je, ninawezaje kuhuisha taarifa za Jina la Biashara kupitia mfumo wa usajili wa ORS?**

Unaweza kuhuisha taarifa za jina la biashara kwa kufungua akaunti kwenye mfumo wa ORS na kuingiza taarifa za jina la biashara husika katika mfumo huo. Taarifa hizo ni pamoja na namba ya usajili wa jina

la biashara, namba ya kitambulisho cha Taifa (NIDA) kwa wamiliki wa sasa, anwani/eneo la biashara pamoja na makazi ya mmiliki, anwani ya barua pepe, namba ya simu ya kiganjani, shughuli zinazofanywa/aina ya biashara na majina ya wanaoendesha akaunti ya benki.

**16. Ninawezaje kufunga jina la biashara?**

Unaweza kufunga jina la biashara kwa kupitia Mfumo wa usajili wa ORS ambapo utatakiwa kujaza fomu Na.7 na kuiwasilisha kupitia mfumo huohuo. Endapo Jina husika la Biashara halijahuishwa katika Mfumo basi fomu Na. 7 ikiwa imeambatanishwa na vyeti halisi vitawasilishwa BRELA kwa ajili ya kufutwa katika daftari la Msajili wa Majina ya Biashara. Maombi ya ufungaji wa Jina la Biashara huambatana na malipo ya ada ya ufungaji wa Jina la Biashara kwa kiasi cha TZS 10,000/=.

**17. Ni namna gani ninaweza kufanya upekuzi wa jalada?**

Upekuzi wa Jalada hufanyika kwa njia mbili: kupitia mfumo wa ORS ambapo baada ya kufanya malipo, unaweza kuomba “standard search” au custom search’; au kutembelea ofisi za BRELA na kufanya upekuzi (perusal) wa jalada husika. Gharama za upekuzi ni kiasi cha TZS 3,000/= Tembelea mfumo wa usajili kupitia https://ors, brela.go.tz au kupitia tovuti ya BRELA www.brela.go.tz na bofya LIMITED COMPANY ONLINE REGISTRATION.

## SEHEMU YA TATU

## MASWALI NA MAJIBU KUHUSU MILIKI UBUNIFU

### A. MILIKI UBUNIFU

Nini maana ya Miliki Ubunifu?

Miliki Ubunifu ni mali au huduma yoyote inayotokana na uwezo wa mtu kufikiria kuanzisha au uvumbua kitu au huduma yoyote mpya yenye au chenye utofauti na ubora zaidi. Ni mfumo unaotambuliwa chini ya mfumo wa sheria za ulinzi wa bunifu mbalimbali.

### MASWALI NA MAJIBU KUHUSU ALAMA ZA BIASHARA NA HUDUMA

### I. ALAMA ZA BIASHARA NA HUDUMA

**1. Nini maana ya Alama ya Biashara na Huduma?**

Ni alama ya kipekee ambayo imebuniwa na mtu kwa madhumuni ya kutofautisha bidhaa anazozitengeneza au huduma anazozitoa na bidhaa au huduma zinazotolewa na watu wengine wanaotengeneza bidhaa au kutoa huduma zinazofanana na za kwake.

Alama ya Biashara au Huduma inaweza kuwa neno, umbo, mchoro, nambari, kifupi cha jina halisi au jina bunifu la mmiliki, kampuni au jina/neno la kubuni isipokuwa yale ambayo yamekatazwa kisheria.

**2. Ni namna gani ninaweza kusajili Alama ya Biashara au Huduma?**

Muombaji anatakiwa kutuma maombi BRELA kwa kupitia Mfumo wa Usajili kwa njia ya Mtandao [Online Registration System (ORS). Mwombaji atatakiwa kwanza kufungua akaunti ambayo atatumia kuingiza taarifa za Alama yake. Ili kutengeneza akaunti kwa Mtanzania anatakiwa kuwa na namba ya kitambulisho cha Taifa (NIDA), barua

pepe, namba ya simu ya mkononi. Kutokana na Sheria jua Alama za Biashara na Huduma wageni hawaruhusiwi kupata huduma ya usajili kwa wao kutuma maombi moja kwa moja bali wanatakiwa kuwasilisha maombi yao kupitia Mawakala wa Alama za Biashara na Huduma waliopo nchini. kwa upande wa makampuni au mashirika mengine yanayoruhusiwa kumiliki alama za Biashara na Huduma yanalazimika kutumia kitambulisho cha NIDA cha mmoja ya wafanyakazi katika taasisi husika.

**3. Ni vigezo gani ambavyo vinahitajika ili kupata Alama ya Biashara au Huduma?**

a) Alama iwe ya kipekee ambayo amebuniwa na mmiliki mwenyewe,
b) Alama hiyo isifanane na alama ambayo ilishasajiliwa na mtu mwingine katika daraja husika,
c) Isiwe na sifa za bidhaa au huduma husika daraja husika na
d) Isiwe kinyume cha sheria na maadili ya Kitanzania.

**4. Je, kuna tofauti gani katika ya Alama ya Biashara na Alama ya Huduma?**

Alama za Biashara zinahusisha bidhaa zinazoshikika mfano nguo, vitabu, machine nk. Alama za Huduma zinahusisha huduma ambazo haziwezi kuonekana kwa macho na hazishikiki mfano wa huduma hizo ni kama vile huduma za kifedha, usafirishaji, bima nk. Kwa kawaida alama za biashara na Huduma zimegawanyika katika madaraja 45 ambayo yametokana na makubaliano yaliyofanyika Nice mwaka 1957 na yanajulikana kimataifa kama "Nice classification- International Classification of Goods and Services".

Kutokana na makubaliano hayo Alama za Biashara ziko kwenye daraja la 1 – 34 na na kwa upande wa huduma ni kuanzia daraja la 35 – 45.

**5. Je, huchukua muda gani ili kukamilisha maombi ya Alama za Biashara au Huduma?**

Maombi ya usajili wa Alama yakishakubaliwa na Msajili wa Alama za Biashara na Huduma, kwa kuzingatia vigezo hutangazwa katika Jarida la Hataza, Alama za Biashara na huduma kwa muda wa siku sitini (60) toka siku ya kutangazwa kwa mujibu wa Sheria, baada ya siku sitini kama hakutakuwa na pingamizi, mwombaji hutakiwa kuwasilisha fomu TM/SM 8 na kulipia ada ya usajili ili kupatiwa cheti cha usajili wa Alama. Hivyo kuanzia kuwasilisha maombi ya usajili wa Alama mpaka kusajiliwa huchukua wastani wa miezi mitatu.

**6. Ni jinsi gani naweza kupata cheti cha usajili wa Alama ya Biashara au Huduma?**

Baada ya kukamilisha malipo ya usajili Cheti cha usajili wa Alama ya Biashara/Huduma hupatikana kwa njia ya mfumo wa usajili wa ORS kupitia account ya mwombaji iliyotumika kupeleka maombi ya usajili wa Alama ya Biashara na Huduma.

**7. Ni namna gani naweza kufanya mabadiliko katika Alama ya Biashara au Huduma?**

kulingana na Kanuni za Alama za Biashara na Huduma Maombi ya mabadiliko yoyote kabla na baada ya usajili wa alama za biashara na huduma hujazwa kwenye fomu husika zinazopatikana katika mfumo wa usajili wa ORS sehemu ya Alama za Biashara na Huduma na kuwasilishwa kwa Msajili wa Alama za Biashara na Huduma kwa ajili ya kufanya mabadiliko na kubadilisha kumbukumbu.

**8. Je, nitawezaje kupata taarifa kama Alama ya Biashara au Huduma imesajiliwa BRELA?**

Taarifa za Alama za Biashara na Huduma zinapatikana kupitia mfumo wa usajili wa Mtandao (ORS). Mwombaji ataingia katika akaunti yake

na kubofya sehemu iliyoandikwa *“information services”* na kuchagua *“standard search”* au *“custom search”* “kama akichagua *custom search”* atabofya tailormade search kisha ataendelea kisha atabofya Alama, upande wake wa kushoto kutakua na box ambalo ataandika jina la Alama pamoja na daraja husika ili kujua kama imesajiliwa au haikusajiliwa. Mwombaji ataendelea kufuata maelekezo mwisho kabisa itampa namba ya kulipia malipo ya huduma hiyo

Akichagua *“standard seach”* atabofya endelea kisha atachagua orodha kisha atabofya proceed ambapo itamlazimu achague aina yadaraja husika ili atumiwe Orodha daraja husika la Nice, baada ya kufanya malipo na kuandika jina la alama ambayo anataka kufahamu kama imesajiliwa pamoja na daraja lake kwa kulipia ada ya Shilingi 10,000/= kisha mwombaji atapata taarifa hiyo kupitia akaunti yake ya ORS moja kwa moja au kutumiwa taarifa hiyo kama alichagua *“custom search-tailor made.”*

**9. Ni sifa zipi zinaweza kuitambulisha Alama ya Biashara au Huduma?**

a) Alama ikubaliane na taratibu za kisheria za usajili wa Alama za Biashara na Huduma,
b) Alama isifanane na alama nyingine ambayo imesajiliwa kwa ajili ya mtu mwingine,
c) Iwe rahisi kusomeka kama ni neno lisiwe na maana ambazo hazikubaliki kisheria na kimaadili,
d) Alama hiyo isielezee sifa au ubora wa bidhaa au huduma inazoziwakilisha na
e) Alama isiwe na viashiria vya udanganyifu wa kijiografia.

**10. Muda gani na Ada kiasi gani itahitajika kuhuisha taarifa baada ya usajili wa Alama ya Biashara au Huduma?**

Baada ya miaka saba toka tarehe ya kusajiliwa kwa Alama ya Biashara au Huduma, mmiliki hutakiwa kuhuisha Alama yake kwa kujaza na kuwasilisha fomu TM/SM 9 na kulipia ada ya Tshs. 30,000/= ya kuhuisha

na TZS 5,000/= ya utunzaji wa kumbukumbu za Alama ya Biashara au Huduma husika, baada ya hapo Alama huhuishwa kila baada ya miaka kumi. Ada ya kuchelewa kuhuisha Alama ya Biashara au Huduma ni TZS 30,000/= ambayo huwasilishwa kwa kujaza Fomu Namba TM/SM 10 na huduma zote hizi zinafanyika kwa njia ya mtandao.

**11. Utaratibu wa kulipia malipo ya Alama ya Biashara au Huduma baada ya muda wake kuisha ukoje?**

Mteja atalipia kwa kupitia mfumo wa usajili wa ORS, ataingia kwenye akaunti yake, ataenda upande wa Alama za Biashara atabofya sehemu iliyoandikwa *"filing of other documents"* na atachagua *"filing type"* hapo anaweza akafanya malipo anayotaka kwa kuchagua fomu aliyoijaza kulingana na anachotaka kulipia.

**12. Baada ya kutuma maombi ya usajili wa Alama ya Biashara au Huduma, Je, ni hatua zipi hufuata hadi maombi kukamilika?**

a) Kwanza maombi yakishapokelewa hufanyiwa uchambuzi wa awali (formality examination).
b) baada ya kufanya uchambuzi wa awali maombi hayo hupewa namba ambayo ndiyo itakuwa namba ya usajili iwapo vigezo vyote vitakuwa vimezingatiwa
c) Maombi haya hufanyiwa ukaguzi wa jina au nembo kama tayari limesajiliwa katika hilo daraja ambalo mwombaji anaomba
d) Baada ya hatua hizo tatu kuisha maombi hufanyiwa uchambuzi wa kina na kutolea mamuzi ya aidha kukubaliwa, kukataliwa, kutangazwa kabla ya uamuzi au kutaka mleta maombi alete uthibitisha wa usajili toka nchi nyingine.

**13. Je, natakiwa kwenda Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) baada ya kupata cheti cha usajili wa Alama ya Biashara au Huduma?**

Hapana

**14. Ni faida zipi naweza kuzipata baada ya kusajili Alama ya Biashara au Huduma?**

a) kuwa na haki ya kipekee kutumia Alama husika na kuwazuia wengine kutumia Alama hiyo isipokuwa kwa ruhusa au ridhaa yako.
b) Kudhibiti ushindani wa kibiashara usiokuwa halali au huduma katika soko.
c) Kuendeleza umaarufu wa ubora wa bidhaa au huduma husika.
d) Kuhifadhi ulinzi wa Alama iliyosajiliwa pamoja na mabadiliko husika.
e) Kumpatia mbunifu wa Alama husika kipato kwa njia ya kuuza Alama au kutoa ruhusa ya matumizi kwa mtu mwingine.
f) Kuwawezesha watumiaji wa bidhaa kutambua na kuchagua alama au huduma kutokana na ubora.
g) Kumpa mmiliki haki ya kisheria itakayompa nguvu ya kumchukulia hatua anayeiga au kutumia visivyo halali alama hiyo.

**15. Ada za Usajili wa Alama ya Biashara au Huduma ni zipi?**

a) Ada ya Maombi TZS. 50,000/=,
b) Ada ya Kutangaza Maombi ya Alama TZS 15,000/=,
c) Ada ya Usajili wa Alama TZS. 60,000/=,
d) Ada ya kutunza Alama (Maintenance Fee) TZS 5,000/=,
e) Ada ya kuhuisha Alama TZS 30,000/=, na
f) Ada nyingine zinapatikana kwenye Kanuni za Alama za Biashara na Huduma za mwaka 2000

## MASWALI NA MAJIBU KUHUSU USAJILI WA HATAZA

## B. USAJILI WA HATAZA

### 1. Nini maana ya Hataza?

Hataza ni hati inayotolewa na Serikali kwa ajili ya kumlinda mvumbuzi

wa teknolojia mpya ya kutatua tatizo la kiteknolojia katika jamii husika. Uvumbuzi huo unaweza ukawa wa kitu kipya kabisa ambacho hakijawahi kuwepo au njia mpya ya kutengeneza kitu chochote chenye manufaa kwa jamii

**2. Je ni vigezo gani vinatumika kwa mvumbuzi kupewa Hataza?**

Ili uvumbuzi upatiwe Hataza teknolojia hiyo ni lazima iwe mpya na iwe haijawahi kutumika mahala popote duniani. Kigezo cha pili ni lazima uvumbuzi huo usiwe unajulikana kabla na usiwe rahisi kwa mtu yeyote mwenye uelewa na Nyanja hiyo kuiga pasipo kutumia akili ya ziada na kigezo cha tatu ni lazima uvumbuzi huo uwe na uwezo wa kutatua tatizo liliokusudiwa kutatuliwa

**3. Je, ni namna gani ninaweza kuomba Hataza?**

Kwanza kabisa kabla hata ya kuanza kutuma maombi BRELA Mwombaji ni lazima ahakikishe ameandaa andiko la uvumbuzi wake kulingana na sheria na kanuni ya sharia za Hataza.

Utaratibu unaotumika kutuma maombi ni kama ilivyoelezwa kwenye utaratibu wa kutuma maombi wa ajili ya Alama za Biashara na Huduma isipokuwa mwombaji atachagua sehemu ya Hataza na atajaza kadiri atakavyokuwa anaelekezwa na mfumo wenyewe.

**4. Ni vitu gani ambavyo vinatakiwa kuwepo kwenye andiko la HATAZA?**

Ili kupata umiliki wa Hataza unahitaji kuandaa vitu vifuatavyo:-

a) Jina la Uvumbuzi,
b) Maelezo ya kina ya uvumbuzi katika nyanja husika yakionesha chimbuko la uvumbuzi huo, Maelezo ya vumbuzi zilizotangulia kwa vumbuzi inayofanania na uvumbuzi mpya, mapungufu ya vumbuzi za awali, Mapendekezo ya namna ya kuziba

mapungufu katika vumbuzi za awali, namana ya utekelezaji wa Uvumbuzi unaokusudiwa

c) Mipaka ya uvumbuzi huo (claims)
d) Dibaji lisilizidi maneno 150
e) Vielelezo kwa njia ya michoro ya Kiufundi (Technical drawings).

**5. Aina gani ya Uvumbuzi inalindwa kisheria?**

a) Uvumbuzi uwe mpya au teknolojia mpya kwenye nyanja husika (novelty).
b) Uwe na kigezo cha uvumbuzi kwenye nyanja husika (inventive step).
c) Usiwe ni uvumbuzi unahusiana na viumbe hai (mimea au Wanyama), usiwe ni nadharia za kihisabati, kisayansi, kiugunduzi au mbinu za tiba.
d) Ukidhi tathmini ya matumizi halisi (industrial applicability).

**6. Aina gani ya Uvumbuzi ambazo haziwezi kupewa Hataza?**

Ugunduzi wa nadharia za kisayansi, Nadharia ya Hesabu, namna ya kutibu binadamu au viumbe hai isipokuwa vifaa au dawa zinazotumika, Mawazo ya aina yoyote ile, matumizi ya mitandao ya Kompyuta, namna ya kucheza michezo

**7. Je, ni gharama kiasi gani inatumika kusajili Hataza?**

a) Ada ya maombi ya Hataza ni TZS 12,000/= na ada ya ulinzi/usajili TZS. 10,000/=,
b) Ada ya maombi ya Uvumbuzi Mdogo (Utility Certificate) ni TZS. 10,000/=, na
c) Ada ya ulinzi/usajili TZS. 8,000/=.

**8. Maombi ya Hataza hushughulikiwa kwa muda gani?**

Kuanzia kuwasilisha maombi ya Hataza mpaka kutolewa cheti ni Siku

120 ikijumuisha siku za kutangazwa katika Jarida la Hataza ambazo ni siku 90 kisheria.

**9. Je, kuna malipo ya kila baada ya muda wa kumiliki Hataza?**

a) Hataza hulipiwa TZS. 4000/= kwa mwaka wa kwanza na malipo haya ni ya kila mwaka kwa kuongezeka shilingi elfu moja kila mwaka mpaka itakapoisha muda wake wa miaka ishirini.
b) Hataza ndogo (Utility Certificate) hulipiwa TZS. 3000/= kwa mwaka wa kwanza na TZS. 1,000/= kila mwaka mpaka itakapoisha muda wa ulinzi wa miaka saba.

**10. Je, Hataza hudumu kwa muda gani?**

Hataza hudumu kwa miaka ishirini (20) kuanzia tarehe ya ulinzi Kwa mchanganuo ufuatao:-

a) Miaka kumi ya kwanza na
b) Kuhuishwa kwa miaka mitano mitano kwa kuwasilisha fomu na kulipia ada ya kuhuisha Hataza.

**11. Ni nini natakiwa kufanya pindi Hataza yangu inapokwisha muda wake?**

Hataza inapokwisha muda wake inakuwa huru (Public Domain) kutumika na mtu yeyote kwa ajili ya biashara ama vinginevyo.

**12. Ni namna gani naweza kupata taarifa za HATAZA ambayo imeshasajiliwa?**

Taarifa za Hataza zinapatikana kwa kuwasilisha maombi kwa njia ya mfumo wa usajili wa ORS sehemu ya “information services” na kupata taarifa zinazoombwa pamoja na kulipia ada husika.

### 13. Kuna Tofauti gani kati ya Hataza na Alama ya Biashara na Huduma?

Hataza ni ulinzi unaotolewa kutokana na uvumbuzi na alama ya biashara ni alama ya kipekee ambayo imebuniwa na mwombaji wa alama hiyo kwa madhumuni ya kutofautisha kati ya bidhaa anazozitengeneza au huduma anayoitoa na bidhaa au huduma za watu wengine wanaotengeneza bidhaa kama zake au wanaotoa huduma kama yake.

### 14. Ni masuala yapi ya kuzingatia kabla na wakati wa kusajili Hataza?

a) Maombi ya Hataza yawasilishwe kabla ya kuchapisha, kutoa muhadhara, kufanya maonesho, kuingia au kusaini mikataba ya matumizi ya uvumbuzi (Non disclosure of invention).

b) Tambua eneo au maeneo ya ushindani wa uvumbuzi au teknolojia husika (commercial value or competitive advantage of patent exploitation).

c) Maombi ya Hataza yanaweza kulindwa kupitia mfumo wa ulinzi wa Hataza kikanda na kimataifa (ARIPO na WIPO PCT Routes).

d) Nyanja ya uvumbuzi inaweza kutumiwa vibaya hususani maangamizi ya ustawi wa jamii [silaha za kibaiolojia mfano kimeta (anthrax) katika vifurushi na barua].

## SEHEMU YA NNE

## MASWALI NA MAJIBU KUHUSU HUDUMA ZA LESENI

### A. LESENI ZA BIASHARA

**1. Je, kwa sasa BRELA ndiyo wanaotoa Leseni zote za biashara nchi nzima?** Hapana, Leseni zinazotolewa na BRELA ni zile za biashara Kundi 'A' tu ambazo zamani zilikuwa zinatolewa na Wizara ya Viwanda na Biashara. Leseni za biashara Kundi 'B' ambazo zinatolewa na Mamlaka ya Serikali za Mitaa bado zinaendelea kutolewa na Mamlaka hizo kwenye kila Halmashauri.

**2. Je, wafanyabiashara ambao wanadaiwa ada Leseni za nyuma zilizotolewa nje ya mfumo wa njia ya mtandao wanalipaje madeni hayo ndani ya mfumo?**

Mfanyabiashara mwenye Leseni iliyotolewa nje ya mfumo wa mtandao na ina madeni ya ada za nyuma na adhabu akiwasilisha maombi kwenye mfumo wa utoaji wa Leseni za biashara kwa njia ya mtandao, kwanza atafanyiwa makadirio ya hayo madeni na kupewa 'control number' kwa ajili ya kulipia madeni hayo tu, kisha atapewa 'control number' nyingine kwa ajili ya malipo ya ada ya kuhuisha Leseni husika kwa mwaka husika.

**3. Kwa mtu ambae ana leseni zilizopatikana nje ya mfumo wa njia ya mtandao anapotaka kuhuisha leseni yake sasa kwa kutumia mfumo wa njia ya mtandao atatakiwa kuleta upya nyaraka zote alizokuwa ameleta awali?**

**Ndio.**
Kwa kuwa mfumo huu wa njia ya mtandao ndio kwa sasa unakuwa kanzi data (database) ya taarifa zote za Leseni za Biashara. Hivyo, taarifa na nyaraka hizo zinaingizwa upya.

**4. Je, naweza kutumia leseni moja hiyo hiyo kwenye maduka yangu mawili ambayo yako kwenye mtaa mmoja?**

**Hapana.**

Sheria ya Leseni za Biashara inataka kila eneo la biashara liwe na Leseni yake ya biashara, hata kama maeneo hayo yapo katika mtaa mmoja.

**5. Ninapaswa kufanya nini ninaposimama kufanya biashara?**

Unapofunga au Kusimamisha biashara, unatakiwa kutoa taarifa kwa kuandika barua kwenye Mamlaka iliyokupa Leseni hiyo (BRELA au Halmashauri husika) kuhusu ufungaji biashara au usitishaji huo ili Mamlaka kuwa na taarifa sahihi.

**6. Je, naweza kulipia leseni ya biashara kwa miaka kadhaa mfululizo?**
**Ndio.**

Sheria inaruhusu mwombaji wa Leseni kulipia ada ya Leseni ya Biashara kwa miaka mitatu mfululizo.

**7. Je, Leseni zote za biashara sasa zinatolewa kwa njia ya Mtandao?**

**Hapana.**
Sio leseni zote zinatolewa kwa njia ya Mtandao kwa sasa. Leseni za Biashara zinazotolewa kwa njia ya mtandao kwa sasa ni Leseni za biashara Kundi 'A' tu zile zinatolewa na BRELA. Taratibu za kiufundi zinakamilishwa ili Leseni za Makundi yote zitolewe kwa njia ya mtandao.

**8. Kuna tofauti gani kati ya Leseni zinazotolewa kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa na zile zinazotolewa na BRELA?**

Leseni zinazotolewa na Mamlaka za Serikali za Mitaa (Halmashauri) ni kwa ajili ya biashara zisizo na sura ya Kitaifa au Kimataifa au

zisizosimamiwa na Sera maalumu ya nchi. Hizi huitwa Leseni za biashara Kundi 'B'
Leseni zinazotolewa na BRELA ni kwa ajili ya Biashara ambazo zina sura ya Kitaifa au Kimataifa au zinazoongozwa na Sera maalumu za nchi.Hizi huitwa Leseni za biashara Kundi 'A'

**9. Mahitaji gani yanatakiwa wakati Kampuni inapoomba Leseni ya Biashara?**

Kampuni inapoomba Leseni ya Biashara hutakiwa kuwasilisha nyaraka zifuatazo:-

a) Cheti cha usajili wa Kampuni (Certificate of Incorporation),
b) Katiba ya kampuni (Memorandum & Articles of Association) iliyokamilika.
c) Endapo wenye hisa wa kampuni wote wako nje ya Nchi, Hati ya Uwakilishi (Powers of Attorney) iambatishwe;
d) Uthibitisho wa mahali pa kufanyia biashara (mf. Mkataba wa pango uliokamilika au Hatimiliki yenye jina la Kampuni inayoomba Leseni;
e) Hati/Namba ya mlipa Kodi (TIN) ya Kampuni ;
f) Vitambulisho vya wenye hisa katika Kampuni (mf. Hati ya kusafiria (Passport), Kitambulisho cha Taifa (NIDA), Kitambulisho cha Tanzania cha kupigia kura au cheti cha kuzaliwa (kwa raia wa Tanzania);
g) Kibali cha kuishi nchini daraja la "A" (kwa wenye hisa wasio Watanzania lakini wanaishi Tanzania).
h) Kibali kutoka kwenye Mamlaka za udhibiti (endapo biashara husika inadhibitiwa na Mamlaka au Sheria maalumu).

**10. Ni mahitaji gani yanatakiwa kuwasilishwa pale mtu binafsi anapotaka kuomba Leseni ya Biashara?**

a) Kitambulisho, kinachobainisha uraia wa mwombaji;
b) Uthibitisho wa mahali pa kufanyia biashara (Mkataba wa

pango uliokamilika au Hatimiliki yenye jina la mwombaji wa Leseni ;

c) Hati/Namba ya Mlipa Kodi (TIN)

d) Kibali kutoka kwenye mamlaka za udhibiti (endapo biashara husika inadhibitiwa na Mamlaka au Sheria maalumu).

**11. Ni mahitaji gani yanatakiwa wakati Kampuni ya Kigeni inapotaka kuomba Leseni ya Biashara?**

Kampuni ya kigeni inapoomba Leseni ya Biashara hutakiwa kuwasilisha nyaraka zifuatazo:-

a) Hati ya uthibitisho wa kuandikishwa hapa nchini (Certificate of Compliance)

b) (Endapo wenye hisa wote wa kampuni wako nje ya nchi, Hati ya Uwakilishi (Powers of Attorney) iambatishwe pia;

c) Uthibitisho wa mahali pa kufanyia biashara (Mkataba wa pango uliokamilika)

d) Hati ya utambulisho wa mlipa Kodi (TIN) ya Kampuni

e) Pass za kusafiria (Passports) za wenye hisa katika Kampuni

f) Kibali cha kuishi nchini cha daraja ya "A" endapo wenye hisa sio Watanzania lakini wanaishi nchini.

g) Kibali kutoka Mamlaka za udhibiti (endapo biashara husika inadhibitiwa na Mamlaka au Sheria maalumu)

**12 Namna gani mwombaji wa Leseni hulipa ada za Leseni za Biashara?**

Ada za Leseni ya Biashara inalipwa baada ya mwombaji wa Leseni kuwasilisha nyaraka za kuomba leseni, kupitiwa na kuidhinishwa na Maafisa Leseni. Zinalipwa kwa kutumia mfumo wa Kielektroniki wa malipo ya Serikali ambapo Mwombaji hupewa hati ya malipo (Invoice) yenye namba ya malipo *"Control Number".* Baada ya kupata hati ya malipo, mwombaji anaweza kufanya malipo kwa njia mojawapo kati ya zifuatazo:-

a) Kulipa Benki moja kwa moja kulingana na jina la Akaunti na la

Benki iliyoelekezwa katika hati ya malipo; au

b) Kulipa kwa njia ya simu za mkononi (Mobile Money) ambapo mlipaji atachagua kulipa malipo ya Serikali, kuingiza namba ya malipo *(Control Number)* na kulipa kiasi kilichoainishwa kwenye hati ya malipo.

**13. Adhabu ya kuchelewa kuhuisha Leseni ya Biashara ni kiasi gani?**

Baada ya tarehe ya mwisho wa uhai wa Leseni husika, Sheria imetoa muda wa siku ishirini na moja (21) kuhuisha leseni, hivyo zikipita siku 21 na muhusika bado hajahuisha leseni hiyo, muhusika atalipa adhabu ya kuchelewa ambayo ni asilimia ishirini na tano (25%) ya ada ya Leseni/biashara hiyo na pia atalipa na ada ya Leseni/biashara husika kwa mwaka huo. . Ikiwa Muhusika ataendelea kuitumia Leseni hiyo bila kuihuisha adhabu huongezeka kwa asilimia mbili (2%) kila baada ya siku thelathini (30) kupita.

**14 Ni utaratibu gani unafuatwa wakati mteja anapotaka kuomba leseni ya biashara katika mtandao? "**

Kwa sasa, Leseni za Biashara za Kundi 'A'; zinaombwa na kutolewa kupitia mfumo wa "The Tanzania National Business Portal" (TNBP). Ili kufanya maombi ya Leseni za Biashara katika mfumo huo mwombaji hufungua tovuti ya www.business.go.tz, kisha bofya palipoandikwa "Services", bofya tena palipoandikwa "Business Licensing Services" kisha endelea kufuata maelekezo ya kufungua akaunti yako na hatimae kujaza na kutoa taarifa za kuombea Leseni utakazoulizwa na kupakia viambatisho vinavyohitajika.

Baada ya kujaza taarifa na kupakia nyaraka/viambatisho, mwombaji hubofya eneo la kuthibitisha usahihi wa taarifa na hatimaye hubofya kitufe cha kuwasilisha ombi husika.

**15. Inachukua muda gani kwa mwombaji kupata Leseni yake ya biashara”**

Kwa mwombaji ambaye amekamilisha taratibu na nyaraka zote zinazohitajika, na kisha kufanya malipo kwa wakati, Leseni inatolewa ndani ya siku moja ya kazi.

## MASWALI NA MAJIBU KUHUSU LESENI ZA VIWANDA NA VYETI VYA USAJILI WA VIWANDA

## B. LESENI ZA VIWANDA NA VYETI VYA USAJILI WA VIWANDA

**1. Ili kupata Leseni ya Kiwanda au Cheti Cha Usajili wa Kiwanda Kidogo ni vitu gani vinahitajika?**

Muombaji anatakiwa kufanya maombi yake kupitia mfumo wa Usajili kwa njia ya Mtandao unaojulikana kama “Online Registration System” (ORS) akijaza taarifa zitakazoulizwa na kuambatisha nyaraka zifuatazo;

a) Mchanganuo wa Mradi (Business Plan)
b) Uthibitisho wa kuwa Kiwanda kipo kwenye eneo lililotengwa kwa ajili ya shughuli za Viwanda [Hati ya eneo (Tittle Deed) au , Mkataba wa Pango (Lease Agreement) au barua kutoka Mamlaka ya Serikali za Mitaa (Local Government Authorities) ambayo kiwanda kipo

**2. Je, kuna gharama yeyote ya kusajili Kiwanda/ Kupata Leseni ya Kiwanda?**

Ndiyo kuna ada zinazolipwa ambazo hutofautiana kutokana na kiwango cha uwekezaji kwenye kiwanda husika kama inavyoonyeshwa kwenye jedwali hapa chini:

| Na. | GHARAMA YA MRADI / UWEKEZAJI | ADA (SHILINGI ZA TANZANIA) |
|---|---|---|
| 1. | Haizidi TZS 5,000,000 | 10,000 |
| 2. | Zaidi ya TZS 5,000,000 lakini haizidi 10,000,000 | 50,000 |
| 3. | Zaidi ya TZS 10,000,000 lakini haizidi 50,000,000 | 100,000 |
| 4. | Zaidi ya TZS50,000,000 lakini haizidi 100,000,000 | 500,000 |
| 5. | Zaidi ya TZS 100,000,000 | 800,000 |

**3. Leseni ya Kiwanda au Cheti cha Usajili wa Kiwanda hudumu kwa muda gani?**

Muda wa uhai wa Leseni hutegemea aina ya Leseni husika;

Leseni ya Kiwanda ya Muda (Temporary Industrial Licence) hudumu kwa kipindi cha miaka mitatu wakati Leseni ya Kiwanda ya Kudumu (Industrial Licence) haina ukomo wa muda.

Cheti cha Usajili (Certificate of Registration) ambacho hutolewa kwa Viwanda Vidogo, hakina ukomo wa uhai. Ni mpaka pale ambapo uwekezaji katika Kiwanda husika utakapo ongezeka na kuwa na sifa ya kupewa Leseni ya Kiwanda.

**4. Nini faida ya kusajili Kiwanda au kuwa na Leseni ya Kiwanda?**

Kusajili Kiwanda kuna faida nyingi zikiwemo:-
Kwa mwenye Kiwanda:-

a) Kutekeleza matakwa ya Sheria ya Taifa ya Usajili na utoaji wa Leseni za Viwanda.

b) Kurasimisha Kiwanda

c) Kupata punguzo la kiwango cha ushuru wa forodha (Import

Duty) wakati wa uingizaji malighafi (raw materials) hapa nchini kwa ajili ya Kiwanda husika.

d) Kumrahisishia upatikanaji wa vibali mbalimbali ambapo Leseni ya Kiwanda ni moja ya kiambatanisho muhimu katika upatikanaji wa vibali hivyo.

**Kwa Taifa**

a) Mapato kwa Serikali yanayotokana na ada za usajili na utoaji wa Leseni hizo.

b) Kuwa na taarifa na takwimu sahihi ya Viwanda pamoja na bidhaa zinazozalishwa ili kusaidia Serikali katika kuweka mipango na Sera madhubuti kwa maendeleo ya Sekta ya Viwanda na Taifa kwa ujumla.

**5. Ni yapi madhara ya kutosajili Kiwanda/ adhabu kwa Kiwanda kisichokuwa na Leseni?**

Kwa mujibu wa Sheria ya Taifa ya Usajili na Utoaji wa Leseni za Viwanda, Sura ya 46 ni kosa kuanzisha ama kuendesha Kiwanda pasipo kuwa na Leseni ya Kiwanda ama Cheti cha Usajili wa Kiwanda kidogo.

**6. Kuna tofauti gani kati ya Leseni za Viwanda na Leseni za Biashara?**

Leseni hizi mbili zinatolewa kwa mujibu wa Sheria mbili tofauti, Leseni ya Kiwanda hutolewa kwa mujibu wa Sheria ya Taifa ya Usajili na Utoaji wa Leseni za Viwanda, Sura ya 46 na ni kwa ajili ya mtu anaetaka kuanzisha kiwanda wakati Leseni ya Biashara hutolewa chini ya Sheria ya Leaseni za Biashara Sura ya 208 na ni kwa ajili mtu anaetaka kufanya biashara. .

**7. Ni mambo gani ambayo mmiliki wa Kiwanda kilichosajiliwa anapaswa kuzingatia baada ya kupata Leseni ya Kiwanda ama Cheti cha Usajili wa Kiwanda kidogo?**

Baada ya kupata Leseni ya Kiwanda au Cheti cha Usajili wa Kiwanda

kidogo, muhusika anapaswa kuzingatia mambo yafuatayo:-

a) Kuwaslilisha kwa Msajili wa Viwanda taarifa za maendeleo ya Kiwanda kila mwaka (Annual Progress Reports)
b) Kuwasilisha kwa Msajili wa Viwanda taarifa za mabadiliko ya kiwanda kama vile kuhamisha Kiwanda kutoka eneo moja kwenda lingine, kuongeza Tawi katika eneo lingine, kubadili umiliki wa Kiwanda n.k.
c) Kuwasilisha kwa Msajili wa Viwanda taarifa za Kuongeza bidhaa ambayo haikutajwa kwenye Cheti/Leseni husika.
d) Kuwasilisha kwa Msajili wa Viwanda taarifa za kufunga kiwanda ama kusimamisha uzalishaji.

Kwa msaada zaidi wakati wa kufanya usajili wasiliana nasi kwa barua *pepe usajili@brela.go.tz* au piga simu kupitia Kituo cha Miito namba 0222 212 800